

FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL10

KISWAHILI PAPER 3 QUESTIONS

SEHEMU YA A (Alama 20)

SWALI LA LAZIMA.

1. a) Maigizo ni nini? (alama 2)
b) Taja vipera vyovyote viwili vya maigizo. (alama 2)
c) Eleza dhima za maigizo. (alama 8)
d) Jadili njia zinazotumiwa na kizazi cha sasa kuendeleza utanzu huu. (alama 8)

SEHEMU YA B (Alama 20)

KIDAGAA KIMEMWOZEA KEN WALIBORA

2. 2. " Naogopa maana aliyemwa na Nyoka akiona ung'ong'o hushtuka.Sipendi kuzungumza kuhusu mambo yaliyotokea,Sipendi kuyazungumzia.Lakini nitakwambia siku.Siku moja nitakwambia.Lakini nitakwambia siku moja.Siku moja nitakwambia.
a) Fafanua muktadha wa dondo hili. (alama 4)
b) Eleza mbinu za lugha zilizotumika katika dondoo hili. (alama 4)
c) Jadili mambo aliyoyaweka siri mnenaji. (alama 12)

AU

3. "Nchi ya Tomoko imejawa na uozo".Tetea kauli hii kwa mujibu wa riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 20)

SEHEMU YA C (Alama 20)

MSTAHIMIKI MEYA

3. "..... wakisubiri ugonjwa nao utasubiri....."
4. a) Faanunua muktadha wadondoo hili. (alama 4)
b) Tambua tamathali mbili za usemi zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)
c) Eleza sifa za mzungunzaji. (alama 6)
d) Eleza umuhimu wa mzungumzaji. (alama 6)

AU

5. Tathmini mbinu walizozitumia wanacheneo kujikomboa. (alama 20)

SEHEMU YA D (Alama 20)

DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE

6. Uhitaji ni mojawapo ya masuala yanayoangaziwa katika diwani ya Damu Nyeusi,eleza.

SEHEMU YA E (Alama 20)

USHAHIRI

7. 1. Naja sas ni ndiyani,naja kwetu mzalendo

Naja nirudi nyumbani, nilowekwa nako kando.

kwetu' mi nakutamani, kulo na mwingi uhondo

Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharani

2 Naja kwingine juwapi, kulojaa langu pendo?

Henda nende kwinginepi, sawa nako kwa muundo?

Kaa kwingine anapi, elewa kwenye lakwe gando?

Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharani.

3 Naja nijie rudi papo, panigendeme mgando

Ningaambiwa kwetu hapo, kwamba kwanuka uvundo

Sitakwenda penginepo, 'tarudi kuko kwa mwando

Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharani.

4 Naja sitapakimbiya, ningambwa kuna vimondo

Takujakuvilekeya, vinanijiya kwa rundo

Nilipozawa 'tafiya, sikimbii kwenda kando

Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharani.

5 Naja hiwa 'mekomaa, kuzidi nilivyo mwando

Tena nnjiandaa, kwa fikira na vitendo

Kwetu nije kuifaa, na kitilioya pondo

Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharani

6. Naja na ingawa maja, siwaekei mifundo

Moyo wangu ushatuja, mawi nalotendwa mwando

Ela wataoningoja, na nyao viwi vitendo

Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharani.

a) Eleza jinsi 'uzalendo' wa mshairi unavyo jitokeza katika beti za 1 na 2. (alama 4)

b) Fafanua jazanda zinazopatikana katika mshororo: Kaa kwingine anapi, ela kwenye gando? (alama 2)

c) Andika ubeti wa tatu katika lugha ya nathari. (alama 4)

d) (i) Katika ubeti wa 5 mshiri amebadilika. Eleza (alama 2)

(ii) Ananua kufanya nini pindi arudipo? (alama 2)

e) Eleza ujumbe unaopatikana katika ubeti wa 6. (alama 2)

f) Andika maneno haya katika Kiswahili sanifu; (alama 2)

(i) Mwando

(ii) ningambwa

g) Kibwagizo cha shairi kinampa sifa gani mshairi? (alama2)

8. VITA VYA NDIMI

Huyo !Amshike huyo!

Hakuna bunduki wala kifami

Bomu na risasi hata hawazijui

Lakini mno wanashambuliana

Kwa ndiMi zilizonolewa kwa makali

Vipande vya matusi silaha zao

Yu imara mmoja wao

Akirusha kombora la neno zito!

Linitingishe adui wake

Na kumgusa hisia kwa pigo kuu

Pigo linalochoma moyoni kama kichomi

Kuchipuza joto la hasira na kisasi

Katika mapigano yaso na kikomo

Filimbi ya suluhu inapulizwa kuwaamua!

Ni nai anayekubali suluhu?

Roho zinakataa katakata

Huku ukaidi ukinyemelea na kutawala kote

Mapandikizi ya watu yakipigana

Vita shadidi visivyo ukomo

Vita vya ndimi!

Magharibi sasa

Jua linapungia mkono machweo

Nalo giza likinyemelea kwa kuburi na

Kasi

Sisikii tena sauti za misonyo
Mate ya watesi yamekakuka

Makanwa yao yamelemewa na uchovu

Sasa wameshikana mikono

Ishara ya suluhu

(a) Hili ni shairi la aina gani? (al.1)

(b) Eleza dhamira ya mshairi. (al.2)

(c) Eleza sifa za utunzi alizotumia mshairi. (al.3)

(d) Taja tamathali zozote tatu alizotumia mshairi. (al.3)

(e) Eleza toni ya mshairi katika beti tatu za awali. (al.1)

(f) Eleza hatima ya yanayozungumziwa kwenye shairi. (al.1)

(g) Mshairi ametumia alama hisi kwingi. Eleza umuhimu wake. (al.1)

(h) Itambue nafsi neni katika shairi. (al.1)

(i) Andika mishororo ya kwanza mitatu ubeti wa 4 kwa lugha ya nathari. (al.3)

(j) Toa maana ya msamiati huu. (al.2)

(i) Kombora

(ii) Misonyo